


# GLOBAL HEALTH/AFYA

# TANZANIA

## AFYA

### TANZANIA

Marekani na Tanzania zimeshirikiana kwa miongo kadhaa kushughulikia mahitaji muhimu ya afya, kwa kuzingatia huduma bora zilizojumuishwa, uimarishaji wa mifumo ya afya, na mienendo ya afya bora. Jitihada hizi zinaunga mkono juhudi za Tanzania za kuboresha mchango wa afya na huduma za afya, ikizingatia ufanisi na uwajibikaji. Mchango wa USAID kwa Serikali ya Tanzania ni pamoja na kufadhili miradi ya kupambambana na VVU / UKIMWI, malaria, kifua kikuu, uzazi wa mpango, afya ya uzazi, lishe, usalama wa afya duniani, na afya ya mama, watoto, na afya ya watoto.

## VVU/UKIMWI

Chini ya Mpango wa Dharura wa Rais wa Marekani wa kupambana na UKIMWI, USAID inasaidia Tanzania kufikia lengo la kufanikisha udhibiti wa janga hili ifikapo mwaka 2020, yaani, asilimia 90 ya watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (VVU) wawe wakitambua hali zao, asilimia 90 ya wale waliopima VVU wawepo kwenye matibabu, na asilimia 90 ya wale walio kwenye matibabu waweze kufubaza VVU. USAID inasaidia miradi inayotoa kinga, matunzo na matibabu ili kufikia lengo la kizazi kisichokuwa na UKIMWI, pamoja na upimaji wa VVU kwa mamilioni ya watanzania, tohara ya hiari kwa karibu wanaume 700,000,

na matibabu kwa watu zaidi ya milioni 1 wenye VVU. Kwa kuongezea, USAID inatoa misaada kwawatoto yatima na watoto walio katika mazingira hatarishi walioathiriwa na janga hilo na walezi wao, kuwaunganisha na fursa za kiuchumi na huduma muhimu za afya.

## MALARIA

Tangia mwaka 2006, USAID imefadhili juhudi zilizo chini ya Mfuko wa Rais wa Marekani wa Malaria (PMI) dhidi ya ugonjwa wa malaria kwa kupitia utumiaji wa vyandarua vyenye dawa, dawa za ukoko zinazo nyunyiziwa ndani ya nyumba, na kuzuia ugonjwa wa malaria wakati wa ujauzito. Kwa kuongezea, PMI inafadhili juhudi zinadhibiti kuenea kwa ugonjwa wa malaria kwa kusaidia ununuaji wa vifaa tiba, dawa ya mseto, uchunguzi wa malaria kwa mgonjwa, matibabu ya malaria kwa mgonjwa, uwezo wa rasilimali watu, upatikanaji wa elimu ya kujikinga na ugonjwa wa malaria, na mienendo mizuri ya kiafya kwa jamii. Kwa kushirikiana na Mpango wa Kitaifa wa Kudhibiti Malaria (NMCP) na Mpango wa Kutokomeza Malaria Zanzibar (ZAMEP), juhudi za PMI katika muongo mmoja uliopita zimewafikia mamilioni ya watanzania kwa kupitia njia mbalimbali za kuokoa maisha na matibabu katika hospitali, vituo vya afya, na kwenye jamii.

## KIFUA KIKUU

Mkakati wa kifua kikuu wa USAID kwa Tanzania unashughulikia changamoto za kiutendaji kuzuia, kugundua, na kutibu ugonjwa huo. Hii ni pamoja na kuboresha upatikanaji wa matunzo ya mgonjwa wa Kifua Kikuu, na VVU, na tiba ya Kifua kikuu sugu kwa kutumia dawa mseto, kuzuia maambukizi na kuenea kwa kifua kikuu, na kuboresha nyenzo za Tanzania za kushughulikia taarifa kwa uhuru na kujitegemea. USAID inasaidia pia ujumuishaji wa huduma za kifua kikuu na VVU katika mikoa yenye vipaumbele, kwa kufanya kazi na vifaa kuanzisha maeneo yenye mahitaji yote ya matunzo na matibabu.

## UZAZI WA MPANGO

Ili kupunguza athari zinazotokana na ukuaji wa haraka wa idadi ya watu kulingana na ukuaji wa uchumi, USAID inasaidia upatikanaji wa hiari wa njia za uzazi wa mpango nchini Tanzania hasa katika vituo vya afya vya umma, kwa kuhakikisha bidhaa za uzazi wa mpango zinapatikana muda wote, na kuongeza uelewa kwa huduma zinazopatikana kupitia maeneo ya kijamii na kibiashara, vyombo vya habari, na kupitia huduma za mkoba. USAID inajumuisha haduma hizi za uzazi wa mpango na huduma zingine za afya ili kutimiza mahitaji mapana ya wateja na kupelekea kupungua kwa vifo vya mama na watoto.

## USALAMA WA AFYA DUNIANI

Katika kuunga mkono Ajenda ya Usalama wa Afya Duniani, ushirikiano wa mataifa zaidi ya 60 waliojitolea kupunguza milipuko ya magonjwa, USAID inafanya kazi na Serikali ya Tanzania kuzuia, kugundua, na kudhibiti magonjwa yanayoambukiza. Kwa kugundua uwezo wa kusambaa kwa magonjwa yanayotokana na wanyama kwa wanadamu, USAID inasaidia mkakati wa "Afya moja" nchini Tanzania, ambao unaunganisha utayari na majibu katika sekta zote pamoja na afya ya umma, dawa ya mifugo, utekelezaji wa sheria, na mazingira / wanyama wa porini.

## AFYA YA MAMA, UZAZI NA MTOTO

# AFYA

## KIWANGO CHA UFADHILI

Dola za Marekani milioni 218.8 kwa mwaka wa fedha 2019

## WATEKELEZAJI WAKUU

- Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto
- Wizara ya Afya, Zanzibar
- Ofisi ya Rais-Tawala za Miko ana Serikali za Mitaa
- Tume ya Taifa ya Kudhibiti UKIMWI•
- Baraza la Watu Wanaoisihi na Virusi Tanzania
- Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Malaria
- Programu ya kutokomeza Malaria Zanzibar
- Mfuko wa kimataifa wa kusaidia mapambano dhidi ya VVU, kifua kikuu au TB na malaria (Global Fund)
- Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF)
- Benki ya Dunia
- Shirika la Afya Duniani (WHO)
- UNICEF

### MAENEO YA MRADI

Nchi nzima

### MAWASILIANO

Laurel Fain

lfain@usaid.gov

### KWA MAWASILIANO ZAIDI

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania

Katika ngazi ya taifa, USAID hutoa msaada wa kitaalamu kuboresha ubora wa miradi ya afya ya mama, uzazi na mtoto Hii ni pamoja na uandaaji wa miongozo ya huduma za kitabibu wakati wa mama kujifungua kawaida, huduma za kujifungua za dharura pamoja na matunzo kwa mtoto mchanga; kusaidia uanzishwaji wa chanjo mpya; na kampeni za kitaifa za mabadiliko ya kitabia kwa malengo ya kutoa taarifakwa kina mama juu ya huduma muhimu za kiafya. Juhudi za hivi karibuni pia zimejikita katika kuunda mfumo wa huduma inayozingatia utu na staha kwa wakina mama hasa wakati wa uchungu na kujifungua.

## UIMARISHAJI WA MIFUMO YA AFYA

Changamoto za mifumo ya afya, kama vile usafirishaji wa vifaa, uhaba wa wafanyakazi wa sekta ya afya, na rasilimali duni za kifedha zinazuia malengo ya maendeleo ya Tanzania. Ili kuboresha utoaji wa huduma na kuunga mkono lengo la Tanzania la huduma za afya kwa watu wote, USAID inafanya kazi na Serikali ya Tanzania kupunguza upungufu ya wafanyakazi wa afya, kuboresha mifumo ya taarifa, na kuongeza upatikanaji wa fedha za ndani kwa kuongeza wigo wa bima ya afya, kuongezeka kwa mgao wa bajeti ya serikali, na ufanisi zaidi wa matumizi ya fedha.